

**OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO**



Telephone: 0262968010
Fax: 0262968010
Website: www.kilolodc.go.tz
Email: ded@kilolodc.go.tz/ded.kilolo@iringa.go.tz

S.L.P2324,
KILOLO
Tanzania .



Kumb. Na. KDC/A.3/20/VOL.II/64

23/07/2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Kwa mujibu wa kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb Na: FA/170/363/01"A"/46 cha tarehe 04/05/2021 cha kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa ya kutuma maombi ya nafasi ya kazi ya Mtendaji wa Kijiji Daraja la III kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyopo katika tangazo hili.

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (VILLAGE EXECUTIVE III) - NAFASI 2:

a) SIFA

- Awe amehitimu Elimu ya kidato cha IV au VI na awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti cha Technician Certificate (NTA level 5) katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wwa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo - Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

b) KAZI ZA KUFANYA/MAJUKUMU

- Atakuwa Mtendaji na mshauri wa Serikali ya Kijiji na Kamati zake katika mipango ya maendeleo.
- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji na atasimamia mapato na matumizi ya Halmashauri ya Kijiji.
- Atakuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- Atapaswa kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango na Maendeleo ya Kijiji.
- Atatafsiri Sera, Taratibu na kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo za Halmashauri ya Kijiji.
- Atakuwa Katibu wa Kamati ya Halmashauri ya Kijiji.
- Ataongoza vikao vya maendeleo ya kijiji vitakavyowahusisha wananchi na wataalam waliopo kwenye eneo lake.
- Atapaswa kuhamasisha wananchi katika mikakati mbalimbali ya kuondoa njaa na umasikini.
- Atakuwa kiongozi wa wakuu waldara na vitengo wa kitaalam katika kijiji

